*SPECIAL REPORT*

# UZINDUZI WA MAWASILIANO TOWERS



Tcra

CREATING A LEVEL PLAYING FIELD



## Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete

Ninakushukuru sa Mheshimiwa Waziri na Uongozi mzima wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kunialika kushiriki au kujumuika nanyi katika uzinduzi wa jengo hili zuri maarufu kama
"Mawasiliano Towers".



*Freq. Management Engineer Jumanne Ikuja briefs the President on Spectrum Analyser and Radiation reader.*

Napenda kutumia nafasi hii kuipongeza Bodi ya Wakurugenzi, uongozi na watumishi wa TCRA kwa kufanikisha ujenzi wajengo hili. Nawashukuru sana wachoraji – rafiki yangu Feruzi tulisoma naye sekondari Kibaha lakini yeye alikuwa mbele yangu na alijua sana hesabu; kwa hiyo sikushangaa yeye
kuishia kuwa architect – kwa kazi nzuri mliyofanya na Mhandisi Mshauri kwa kazi nzuri uliyoifanya. Tunawashukuru wajenzi kampuni ya Kichina waliojenga jengo hili kwa kujenga jengo zuri ambalo kama walivyosema wasemaji walionitangulialimependezesha sana mandhari ya eneo hili.

Wakati mwingine nimekuwa najiuliza na ndio maana nilikuwa nazungumza sana, ni vizuri watu wa jiji nao wakapangapanga vizuri maeneo yao. Sasa ukishakuwa kuna jengo hili ni lazima eneo hili sasa lipate majengo yanayofanana na haya, lakini mnatoa kbali cha kujenga jengo hapa halafu mnatoa kbali cha kujenga – mnaweza kupina na viwanja vya nyumba za vyumba sita. Hapa patakuwa mahali hapapendezi. Sasa ni vizuri, wakaona kwamba maadamu kuna hili, mbele pale kuna Mlimani City, wakiona namna pia ya kuibadilisha masterplan ya eneo hili ifanane na mazingira halafu kukawa na eneo moja hivi zuri katika jiji. Lakini nimefurahi kwamba katika maelezo yenu kwamba jengo hili pia limejali ndugu zetu wenye ulemavu wa viungo ambao wanaweza kuingia kwenye jengo hili kwa urahisi na hayo ndiyo mahitaji ya ujenzi kwa siku hizi.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza sana TCRA kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mnaifanya toka muasisiwe. Waziri ameeleza vizuri, Mwenyekiti wa Bodi na Mkurugenzi Mkuu wameeleza kwamba kazi yenu nzuri imetambuliwa. Waswahili wanasema 'chanda chema huvishwa pete' na ninyi mmepewa tuzo ya kutambua kazi nzuri mnayofanya, kuwa Mamlaka Bora ya udhibiti wa Mawasiliano mwaka 2009 kwa eneo la Afrika kusini mwa jangwa la Sahara. Sio jambo dogo, ni jambo kubwa.

Nawapongeza sana kwa kazi hii nzuri. Lakini isiwe ile ya 'mgema ukimsifia tembo hulitia maji'. Endeleeni na moyo huo huo ili muendelee kuonekana na kuendelea kupata tuzo. Hata kama hamkupata tuzo, muendelee kuonekana kama mnafanya kazi zenu vizuri; maana hatufanyii tuzo, tunafanya kazi hizi kwa ufanisi wetu na hivyo mkifanya hivyo kama taaasisi tutafurahi sana hivyo.
Kutokana na kazi nzuri mnayoifanya, sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha sana. Mkurugenzi Mkuu umeeleza vizuri kwamba simu za mkononi zimeongezeka zimefikia sasa zaidi ya laini milioni 20.5 zimegawiwa, watumiaji wa intaneti wameongezeka wamefikia mjkilioni 4 laki nane. Haya sio maendeleo madodo; ni makubwa sana. Katika Afrika sisi ni miongoni mwa nchi ambazo upanuzi wa sekta ya mawasiliano unakuwa sana, hasa matumizi ya simu za mkononi. Nadhani kwa Afrika wanaoongoza ni Nigeria. Lakini pia imeelezwa vizuri kuwa katika simu hizi hata huduma zimeongezeka, maana sio tu kwamba simu zinatumika kwa kuongea – mfano mtu kupiga kijijini kuulizia hali – lakini pia huduma zimeongezeka, watu wanatuma pesa. Watu wanalipa bili za huduma kupitia simu. Unaweza kupokea intaneti kwenye simu yako.



*Former TCRA Director Generals, Board Chairman and other officials.*

Kwa hiyo haya ni maendeleo makubwa. Lakini maendeleo haya hayawezekani kama facilities zenyewe haziwezi kuwepo. Kwa hiyo kazi kubwa inafanywa. Hivyo Hongereni sana; tunataka muendelee. Lakini sisi katika serikali tunatambua kwamba huduma ya mawasiliano hii itanufaika zaidi kama kutakuwa na mtandao unaotumia nyaya za optic fibre. Kwa kutambua hivyo ndiyo maanda tumefanya uamuzi mgumu, wa gharama kubwa, wa kuwekeza katika mkongo wa taifa. Tumetambua kwamba ndiyo manufaa yenyewe. Hivyo tumewekeza na tunataka kujenga mkongo wa taifa kilometa zaidi ya 8,000 tufike katika kila wilaya. Kazi hiyo imeanza na inaendelea vizuri. Tumeshafikisha kilometa 4,800 na kazi inaendelea na ahadi niliyokuwa nimepewa ni kuwa ikifika Juni mwaka huu utakuwa umefika kila wilaya. Kwa hivyo tuendelee zaidi. Faida yake tutaiona. Gharama za mawasiliano zitashuka zaidi. Mkitumia satelaiti, gharama zinakuwa kubwa. Lakini sio hivyo tu, mkongo huo wa taifa unaunganishwa na ile super highway ya submarine cable iliyokuwa huko baharinbi – ya SEACOM na nyingine ye Eassy – na mingine itakuja. Hii yote inatusaidia kujenga uwezo mkubwa – uwezo mkubwa sana wa mawasiliano; na mawasiliano yanasaidia sana kukuza maendeleo. Mtu aliyeko Malinyi halazimiki kuja Dar Es Salaam kumwambia mnunuzi kuwa mpunga uko tayari aje kununua. Akiwa pale pale anaweza kupiga simu na kumwambia 'ziko gunia 100 tayari, tuma gari'. Na pengine huyu aliyeko Dar Es Salaam anamwambia mtu aliyeko Ifakara ' nenda Malinyi kwa mzee fulani kachukue magunia yangu 100 uniletee ukifika hapa nitakulipa'. Kwa hivyo inasaidia. Ni kichecheo cha haraka sana cha maendeleo.

Ndio maana tumewekeza sana kwenye eneo hili. Tumetumia pesa nyingi kwa ajili ya kuwekeza. Lakini ni matumaini yetu ni kwamba tukishawekeza kwenye eneo hiloi, mkongo ukishakuwepo, mawasiliano yatakuwa rahisi zaidfi Tutaanza kutumia mkongo kufanya shughuli za serikali kupitia mtandao ( e-government). Kwa mfano mtu aliyeko Namtumbo hana haja ya kuja Dar Es Salaam. Palepale nyumbani kwake, akiwa na kompyuta ndogo anaweza kufikia ofisi ya huduma Dar Es Salaam. Fomu iliyoko pale ataipata, ataijaza, ataituma na mambo yake yatamalizika yuko palepale nyumbani kwake.




*The Director Postal Affairs Mrs. Rehema Makuburi briefs the President on Postcode Project.*

Itatupunguzia ulazima wa watu kwenda kuwaona maofisa; amwambie ' sijaamka, chai sijanywa'. Kwa hiyo hayo yote tunayalenga. Lakini pia tunalenga katika ellimu kwa mtandao (e-education). Tuna mpango mkubwa wa kutumia tekinolojia ya habari kwenye mradi mkubwa sana wa Tanzania Beyond Tomorrow. Tunataka kutumia tekinolojia ya habari kufundishia; tekinolojia ya habari vijana kupata elimu. Mwalimu mmoja anaweza kufundisha kemia nchi nzima kwa wakati mmoja. Ndio maana tumesema kwenye maeneo yote ambako mkongo unapita lengo ni kuunganisha shule zilizokuwepoi kwenye mkongo wa taifa ili siku moja kwa kutumia mpango tuliokuwa nao na tunaouendeleza hivi sasa tuweze kutumia tekinolojia hii ya habari na mawasiliano kwa ajili ya elimu ya watoto wetu. Lakini pia tutaitumia kwa ajili ya tiba – kwamba leo daktari aliyeko John Hopkins Medical School ya Marekani anaweza kuongoza operesheni katika hospitali ya Muhimbili kwa kutumia mawasiliano haya. Kwa hiyo ni kitu ambacho tumekiwekea mkazo mkubwa.

Mwaka juzi nilikwenda Marekani; shabaha yangu ilikuwa ni hiyo tu. Nilikwenda Stanford University kwa sababu wao ndio waliojenga Silicon Valley. Nimetembelea Silicon Valley – makamapuni makubwa ya IBM, Cisco, Google na wenzao; yote kwa nia ya kuwashawishi waje; na Chuo Kikuu cha Stanford kuwaomba waje

watusaidie kulea na kukuza tekinolojia ya habario kwenye vyuo vyetu vikuu vya Dar Es Salaam na Dodoma. Kwa hiyo tujenge huo msingi, ili kesho na kesho kutwa na sisi tujenge Silicon Valley. Na sisi tunaweza kuwa na Chamwino Valley kwa kutumia Chuo Kikuu Dodoma kwa ajili ya kujenga hayo. Kwa hivyo kwa upande wa serikali tuko makini katika kutekeleza hili kwa kutambua umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo nawashukuru sana mnafanya kazi nzuri, kazi kubwa, mmepata mafanikio mazuri. Lakini jingine ambalo tumelifanya katika serikali ni kuanzisha Mfuko huu wa Mawasiliano kwa Wote. Tunatambua kwamba serikali imeacha hii biashara. Lakini imeiacha mikononi mwa sekta binafsi. Sekta binafsi wao watakwenda zaidi kwenye maeneo yao. Kwa hiyo maeneo mazuri yatakuwa Mwanza, Dar Es Salaam, Arusha, Mbeya

– kwenye miji mikubwa. Lakini ukamwambia huyu sasa aende kule Mnacho kule Ruangwa – taabu sana kwenda. Hakuna biashara. Lakini tunataka watu wa kule Ruangwa nao waweze kupata mawasiliano. Kwa hiyo tumebuni huo mfuko wa mawasiliano. Kupitia mfuko huo sasa, tutawezesha makampuni haya, kwa kugharamia sisi, waweze kuzijenga hizi huduma kule kwa wananchi vijijini nao waweze kuwasiliana. Mimi nikizunguka huko vijijijini kilio ni 'mtandao,mtandao'.




*TCRA Board Members, management and other delegates during the event.*




*A Member of the organising committee and ushers pose for photograph in their special attire.*

Nilikuwa ninawakumbusha, nilikwenda wilaya ya Kilindi wakati mmoja, kila unaposimama – kuna kijiji kimoja kinaitwa Kingunde nadhani – pale nimesimama pale kwenye mkutano nikaambiwa "unavyowaona hapa, hawa watu wote kila mtu ana simu ya mkononi, ziko simu zaidi ya elfu hapa. Lakini ama wapande juu ya mti – sasa mwenyekiti wa kijiji ananiambia ' mimi mama mwenyekiti wa kijiji hiki, akina baba wanaweza kupanda, mimi naweza?' ". Kwa hiyo unakutana na madai haya. Mwenyekiti akawaambia wananchi ' toeni simju zenu juu', nusu ya ule mkutano. Kila mtu ana simu yake ya mkononi lakini hawana uwezo wa kuitumia pale, wakienda Gairo kupeleka maharage – maana hayo maharage mnayoyaona njiani, hata mahindi Kibaigwa, viazi Mtumbatu – vinatoka kule; ndiko vinapolimwa. Lakini simu hizi hazipo.

Hivyo kuna mahitaji makubwa sana na ndio maana na sisi pia tukabuni njia za kusaidia pale wawekezaji wanaposhindwa na sisi tutoe mchango. Lakini kila jema halikosi changamoto zake. Mkurugenzi Mkuu ameeleza vizuri sana changamoto mbalimbali zilizokuwepo. Ameelza vizuri – maana kuna mahali pengine kazi yao wanakuorodheshea changamoto tu; kwamba wewe mgeni rasmi ndio una majawabu ya hizo changamoto zao.
Lakini uzuri wa wenzetu hawa wameeleza changamoto lakini pia wameeleza majawabuy walivyojipanga kukabiliana nazo na zile ambazo zinahiotaji msaada wa serikali wamezitamka vizuri. Na mimi nataka kuwahakikishieni kwamba yale ambayo ni wajibu wa serikali tuleteeni, tutayafanyia kazi.

Katika changamoto nilimkumbusha mwenyekiti na baadae nikamkumbusha waziri, hamkuitaja moja – ya matumnizi mabaya ya mawasiliano hayo. Hiloi hakuna msimamizi mwingine isipokuwa nyie. Hili msilizungumze kwa kuumauma meno – hapana! Huko duniani ni mojawapo ya changamoto kubwa. Pornography wanapambana nayo sana. Madude haya kutumika kwa ajili ya kufanikisha vitendo vya kiigaidi, ni kazi ya mamlaka.
Hivyo jambo hili msilizungumze kwa kuumauma meno. Ni jukumu lenu! Simamieni. Isije tekkinolojia ya habari ikatumika kuharibu maadili ya taifa;ikatumika kwa ajili ya kufanikisha uhalifu. Hili jambo lazima mlizungumze wazi; msiwe na kigugumizi nalo!

Uhuru utakaomong'onyoa maadili ya watoto wetu sio uhuru. Hauna faida. Hata huko wakuu wale wa demokrasia kwelikweli hili hawakubali kabisa. Jamii inalo jukumu la kuilea jamii yake. Msilee watoto ambao huko mbele ya safari ni wazungu wa unga, watu wanaofanya mambo ya ovyo ovyo katika jamii kwa sababu wamewezeshwa kufanya hivyo kupitia intaneti na kupitia simu za mkononi.

Tusiruhusu kutumia simu ya mkononi kutukana watu. Ni wajibu wenu. Hakuna mtu mwenye maadili mema anatukana mwenzake. Kwa hiyo ni lazima hili mlisimamide maana nimesikiliza changamoto zote hili sikulisikia. Msiwe na kigugumizi nalo. Tusiache jamii hii ikamong'onyolewa kwa kutumia jambo hili jema ambalo linaweza kufanikisha maendeleo ya taifa letu.

Endeleeni kugawa masafa. Endeleeni kuwabana wale ambao wanahodhi masafa; hawayatumii. Yote haya mnajua namna ya kuyafanya.
Kwa hiyo nimalize kwa kusema kwamba nashukuru; nimefurahi kualikwa na kushirikishwa kwenye shughuli hii. Ninawapongezeni kwa mafanikio haya makubwa. Nawapongezeni kwa mafanikio niliyoyaona pale juu. Vitu vyenyewe vidogo lakini mambo yake makubwa. Lakini hayo ndiyo mabadiliko yenyewe. Maana zamani kompyuta ulikuwa unahitaji jengo zina hili. Kulikuwa kuna mitambo tu; sasa hivi hali imebadilika.

Safari moja nilikwenda kiwanda cha Sun Flag pale Arusha wakanionyesha mitambo yao ya zamani na mitambo yao ya sasa. Ile ya zamani imechukua nafasi kubwa kwelikweli. Hii ya sasa imechukua nafasi ndogo lakini uwezxo wa hii ya sasa ni mara elfu ya ile mikubwa. Lakini ndiyo maendeleo ya tekinolojia yanavyokwenda. Hata simu za mkononi, tulipoanza, simu za kwanza zilikuwa mzigo, lakini sasa hivi zinazidi kushuka tu. Nadhani baada ya miaka michache ijayo tutakuwa na 'miniature phones'.
Kwa hiyo kuna mafanikio makubwa, tunaendelea vizuri na sisi tunasonga mbele. Napenda kuwatia moyo, mnafanya kazi nzuri, endeleeni kufanya kazi hiyo, ongezeni bidii, tuisimamie sekta yetu hii ikue vizuri ili tuweze kupata mafanikio makubwa zaidi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yetu.

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI, NA TEKINOLOJIA MHESHIMIWA PROFESA MAKAME MBARAWA (MB)

Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii ya pekee kukushukuru wewe Mheshimiwa Rais kwa kukubali kujumuika nasi katika hafla hii ya ufunguzi wa jengo la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Mawasiliano Towers.

Sisi viongozi wa Wizara pamoja na viongozi wa mamlaka ya Mawasiliano tumefarijika sana kwa uamuzi wako wa kujumuika nasi siku ya leo pamoja na kuwa tunajua una majukumu mengi ya kitaifa lakini umeweza kupata fursa ya kufika hapa. Tunakushūkuru na karibu sana.



*President Kikwete presses an alarm in symbolic launch of the 14 storey Mawasiliano Towers built at the cost of 39bn/=. It is now one of the sources of income for the government.*


Kwa kuzingatia program ya shughuli zetu hapa leo, jukumu langu kubwa ni kukukaribisha wewe mwenyewe Mheshimiwa Rais kutuzindulia jengo letu la Mawasiliano Towers ambalo limejengwa kwa fedha zetu sisi wenyewe. Hata hivyo kabla ya kukukaribisha Mheshimiwa Rais, naomba nizungumze masuala machache yanayohusu sekta ya mawasiliano.

Kwa kipindi kifupi nilichokaa katika wizara hii baada ya kuniteua mwezi Novemba 2010 nimepata fursa ya kufahamu masuala kadhaa kuhusu sekta ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto mbalimbali za sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Rais, chini ya uongozi wako umekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba sekta ya mawasiliano inchangia vyema katika kuleta maendeleo hapa nchini. Hii inajidhihirisha katoka kuipatia sekta ya mawasiliano kipaumbele katika sera, mikakati na sheria mbalimbali za sekta. Sera za mawasiliano, sera za TEKNOHAMA, Sera za Utangazaji na Posta,Sheria ya Mawasiliano ya Elektroniki na Posta na kanuni zake ambazo zitakamilishwa hivi karibuni ni baadhi tu ya sera na sheria muhimu ambazo umehamikisha kamba zinapata nafasi stahili katika utekelezaji wake ili sekta ya mawasiliano iweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya taifa letu.

Sera na kanuni hizi zimekuwa chachu ya maendeleo ya sekta na uchumi kwa ujumla kwa kuwa zimeweza kuweka mazingira mazuri ambayo yataiwezesha sekta kusonga mbele. Matokeo yake makampuni ya ndani na nje yameweza kuwekeza katika sekta ya mawasiliano na TEKNOHAMA hapa nchini. Umekuwa ukifanya hivyo kwa kusudi la kuhakikisha kuwa nchi yetu haibaki nyuma katika suala zima la teknolojia ya habari na mawasiliano duniani.

Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 iliweka bayana mikakati ya maendeleo ya sekta ya mawasiliano nchini na kutamka bayana kuwa itafanya jitihada za makusudi katika kuboresha sekta ya mawasiliano ili kila raia wa nchi hii aweze kupata mawasiliano yaliyo bora na kwa bei nafuu.
Hakika katika kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya serikali ya Awamu ya Nne unayoiongoza, sekta ya mawasiliano imekuwa ikikua kwa kasi na kuongeza pato la taifa, ajira na kurahisisha maisha wa watanzania katika shughuli zao za kila siku.



*TCRA Officers during the launch.*

Itakumbukwa Mheshimiwa Rais, wakati wa ziara zako mbali mbali ndani na nje ya nchi umekuwa ukiwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika sekta mbali mbali ikiwa ni pamoja na sekta ya mawasiliano. Tuna kila sababu za kukushukuru, Mheshimiwa Rais, kwa umuhimu uliouweka katika kuendeleza sekta ya mawasiliano nchini katika kipindi chote cha uongozi wako tangu uingie madarakani.
Kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika kusimamia sekta hii imewezesha kupatikana maendeleo makubwa katika sekta na utendaji bora unaoweza kuigwa na wengi.
Usimamizi mzuri wa sekta ya mawasiliano nchini umewezesha wawekezaji kuwa na imani ya kuwekeza hapa nchini na ndiyo maana tumekuwa nchi pekee na ya kwanza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na makampuni mengi ya mawasiliano baada ya kufungua milango ya uwekezaji wa sekta ya mawasiliano.

Mara kadhaa taasisi na nchi marafiki zimekuwa zikiomba wataalamu wao kuja kujifunza kutoka TCRA ili kuelewa jinsi ya kusimamia sekta ya mawasiliano kwa ufanisi zaidi. Hata katika nyanja za kimataifa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni Mamlaka inayoheshimika na kuaminika sana. Tanzania, kupitia Mamlaka hii,imekuwa moja ya wajumbe wanne kutoka Bara la Afrika wa Baraza la Baraza la Uongozi la Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia mawasiliano ulimwenguni (ITU) kuanzia 2006 hadi 2010. Aidha, kutokana na utendaji mzuri wa Mamlaka hii, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilichaguliwa kuwa ni mamlaka bora (best regulator) wa masuala ya mawasiliano barani Afrika kwa mwaka 2009.

Ni dhahiri kwamba utendaji mzuri wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania unatokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na sera, sheria na kanuni za nchi yetu ambazo wewe Mheshimiwa Rais ndiye msimamizi mkuu.

Wawekezaji katika sekta na watumiaji wa huduma mbalimbali za mawasikliano wamepata uhakika (confidence) katika kuwekeza na pia katika kutumia huduma za mawasiliano. Palipo na mafanikio hapakosi changamoto.

Ninaamini kuwa Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Tekinolojia kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya mawasiliano tutaendelea kushirikiana kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo ili sekta ya mawasiliano iweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya nchi yetu.

Ujenzi wa jengo hili na kukamilika kwake kunaonyesha jinsi TCRA ilivyoweza kulenga mbali. Pamoja na kukidhi mahitaji ya kiofisi ya TCRA, jengo hili limekuwa kivutio katika mandhari ya jiji letu na pia linachangia katika pato la taifa letu ikiwa ni pamoja kuongeza ajira na wawekezaji kupata sehemu ya kuweka ofisi zao na hata kufanyia vikao na mikutano mbali mbali.

## HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA MHESHIMIWA JAJI CHIPETA (MSTAAFU)



Kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii ya pekee kukushukuru kwa kukubali mwaliko wa kuja kuzindua jengo la Mawasiliano Towers. Karibu sana Mheshimiwa Rais.

Pili naomba nitoe shukrani za dhati kwa viongozi wa kitaifa wa serikali na taasisi mbalimbali kwa kuitikia mwaliko wetu huu.
Jukumu langu ni kumkaribisha Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya sekta ya Mawasiliano nchini ili aseme machache na kukukaribisha uzungumze nasi na hatimaye kuzindua jengo letu.

Kabla sijafanya kazi hiyo, naomba niseme machache kama ifuatavyo;

- Bodi imekuwa ikitoa maamuzi juu ya maombi ya leseni mbali mbali za masuala ya mawasiliano nchini;
- Bodi imekuwa ikipokea mawazo na ushauri kutoka kwa wadau wa mawasiliano na kuyafanyia kazi pamoja na kutoa maamuzi;
- Bodi kwa kupitia Kamati ya Malalamiko na Kamati ya Maudhui, imekuwa ikiyafanyia kazi mala lamiko kutoka kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano nchini na kutoa uamuzi kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa;
- Bodi pia imekuwa ikisimamia utendaji wa Menejimenti ya Mamlaka ya Mawasiliano kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo;
- Bodi hii ndiyo iliyofikia maamuzi ya ujenzi wa jengo hili linalopendeza katika mandhari haya.

Kuhusu uamuzi wa ujenzi wa Mawasiliano Towers, nashukuru kwamba Serikali iliridhia tulipowasilisha mchanganuo wa mradi kwa ajili ya kibali cha utekelezaji wake. Ridhaa hiyo iliipa imani bodi kufanya kazi zake kwa uaminifu mkubwa.
Sisi Wakurugenzi wa Bodi ya Mamlaka tuna kila sababu ya kuwapongeza watoa huduma wa sekta ya mawasiliano kwa kuwa karibu nasi katika mawazo na ushauri pale tunapokutana nao katika mikutano na semina mbali mbali.

Kukamilika kwa ujenzi wa jengo hili kumeleta ufanisi mkubwa katika sekta ya mawasiliano, tofauti na siku za nyuma ambapo huduma zetu zilikuwa zikitolewa katika majengo mawili tofauti ya Mikocheni na Upanga.

# HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, PROFESA JOHN NKOMA

Napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kukushukuru wewe **Mheshimiwa Rais** kwa kukubali kuwa mgeni rasmi na kushirikiana nasi katika shughuli hii muhimu ya uzinduzi wa jengo letu jipya la Makao Makuu ya Mamlaka ya Mawasiliano nchini, liitwalo **"Mawasiliano Towers".**

Tunafahamu wingi wa kazi zako na ugumu wa ratiba yako ya kazi na majukumu ya kitaifa ulionayo lakini umeweza kuja kushiriki nasi. Kushiriki kwako katika hafla hii, kumetufariji mno kwani ni kielelezo thabiti cha imani yako kwetu na kuthamini tukio hili muhimu katika historia ya Mamlaka ya Mawasiliano nchini.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communications Regulatory Authority – TCRA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya mwaka 2003. Mamlaka ilichukua majukumu yaliyokuwa yakisimamiwa na zilizokuwa Tume ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communications Commission – TCC) na Tume ya Utangazaji Tanzania (Tanzania Broadcasting Commission – TBC).

Kuunganishwa kwa taasisi hizo mbili kulitokana na uamuzi wa serikali ili kwenda sambamba na maendeleo ya kiteknolojia katika sekta ya mawasiliano. Mamlaka hii inahusika na udhibiti wa simu, utangazaji, posta na teknolojia za elektroniki, na kwa ujumla matumizi ya simu, televisheni, radio na kompyuta ikiwemo intaneti.



*TCRA DG shakes hands with President Kikwete as he departs after the inaugural event launch.*

### Wajibu na MAJUKUMU ya TCRA ni kama yafuatavyo:

- Kukuza ushindani katika utoaji wa huduma za sekta ya mawasiliano na utangazaji nchini;
- Kulinda maslahi ya watumiaji huduma za habari na mawasiliano nchini;
- Kuweka mazingira yatakayosaidia watoa huduma waweze kunufaika na uwekezaji ;
- Kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia watumiaji wote wakiwemo wa kipato cha chini, walio viji jini na wasiojiweza; kuelimisha umma ili uelewe vema huduma zinazotolewa katika sekta;
- Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na 12 ya 2003;
- Kutoa leseni na pia kufuta inapobidi kwa kuzingatia maelekezo ya Sheria ya Sekta inayohusika;
- Kuweka vigezo na kusimamia utoaji wa huduma za mawasiliano, Posta na Utangazaji ;

- Kusimamia utendaji wa watoa huduma katika sekta ikiwa ni pamoja na viwango vya uwekezaji; gharama za huduma; ubora wa utoaji na usambazaji wa huduma, n.k.;
- Kusuluhisha migogoro na malalamiko ndani ya sekta;
- Kutunga sheria ndogo na kanuni zitakazorahisisha utekelezaji wa Sheria ya Mamlaka pamoja na zile za sekta;
- Kushirikiana na wadhibiti wa mawasiliano katika nchi nyingine ili kuboresha utoaji huduma nchini;
- Kuzingatia mikataba iliyowekwa baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali nyingine au Mashirika ya Kimataifa;
- Kutelekeza majukumu mengine itakayopangiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

## SERA, SHERIA, KANUNI NA MFUMO WA LESENI

Sekta ya Mawasiliano imekuwa haraka sana na mojawapo ya sababu ya maendeleo hayo ni kuwepo kwa sera, sheria, kanuni na mfumo mzuri wa utoaji leseni.

SERA (COMMUNICATION POLICIES)

Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya simu ya mwaka 1997 (National Telecommunications Policy of 1997)
Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003 (National ICT Policy of 2003)
Sera ya Taifa ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 (National Information and broadcasting Policy of 2003)
Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003 (National Postal policy of 2003)

## SHERIA (COMMUNICATIONS LEGISLATIONS)

Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 (Tanzania Communications Regulatory Authority Act No 12 of 2003)

Sheria ya Mfuko wa Mawasialiano ya mwaka 2006 (Universal Communications Service Access Fund Act of 2006)

Sheria ya mawasiliano ya elektroniki na posta ya mwaka 2010 (Electronic and Postal Communications Act (EPOCA) of 2010) ambayo ilipitishwa na Bunge Januari 2010 na kufuta sheria mbili: Sheria ya Utangazaji Na. 6 ya Mwaka 1993 (Tanzania Broadcasting Services Act No 6 of 1993) na Sheria ya Mawasiliano Tanzania Na. 18 ya mwaka 1993 (Tanzania Communications Act No 18 of 1993)



*TCRA DG briefs the President, left, TCRA Board Chairman Judge Buxton Chipeta (RTD).*

## KANUNI (COMMUNICATIONS REGULATIONS)

Kwa hivi sasa kanuni zinazotumika ni za mwaka 2005. Ili kwenda na wakati, na kufuatana na sheria mpya ya EPOCA, mchakato unaendelea ili kutengeneza kanuni mpya za mwaka huu 2011. Wadau wote wa sekta watahusishwa. Kanuni hizi mpya zitazingatia maendeleo kwenye sekta. Kanuni za mwaka 2005 ni hizi zifuatazo:




*TCRA Corporate Communications Manager Mr. Innocent P.M Mungy addresses delegates as he co-ordinates the launch event .*

- The Tanzania Communications (Broadband Service) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Consumer Protection) Regulations 2005
- The Tanzania Broadcasting Services (Content ) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Licensing) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Importation and Distribution) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Installations and Maintenance) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Interconnection) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Telecommunication Numbering and Electronic address) Regulations 2005
- The Tanzania Postal Regulations 2005
- The Tanzania Communications (RadioCommunications and Frequency Spectrum ) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Tariff) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Type Approval of Electronic Communications Equipment) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Quality of Service) Regulations 2005
- The Tanzania Communications (Access and Facilities) Regulations 2005

## MFUMO WA LESENI (CONVERGED LICENSING FRAMEWORK)

Tarehe 23 Februari, 2005, Mamlaka ilianzisha mfumo mpya wa utoaji leseni unaozingatia muingiliano wa teknolojia unaojulikana kama "Converged Licensing Framework" (CLF). Leseni zinazotolewa katika mfumo huu hazifungamani na aina ya teknolojia inayotumika (Technology Neutral) wala aina ya huduma inayotolewa (Service Neutral). Zipo aina nne za leseni zinazotolewa katika mfumo huu mpya ambazo ni:

- Leseni ya kujenga miundo mbinu ya mawasiliano (Network Facilities License (NFL))
- Leseni ya kutoa huduma za mawasiliano (Network Services License (NSL))
- Leseni za matumizi ya kutoa huduma za mawasiliano (Applications Service License (ASL))
- Leseni ya Utangazaji (Contents Services License (CSL))

Kuna masoko manne: Kimataifa (International), kitaifa (National), kimkoa (Regional) na kiwilaya (District).

Aina nyingine ya leseni zinazotolewa ni:

- o Leseni kwa ajili ya utoajiwa huduma za posta kwa Uma (Public Postal License)
- o Leseni kwa ajili ya utoaji wa huduma za nyaraka na vipeto kwa njia ya haraka (Courier Services License)
- o Leseni kwa ajili ya kutumia ya masafa ( Frequency user License)
- o Leseni kwa ajili ya kufunga na kutengeneza mitambo ya mawasiliano (Installation and Mainte nanceLicense)
- o Leseni kwa ajili ya kuagiza na kusambaza vifaa vya mawasiliano (Importationand and distribution License)
- o Leseni kwa ajili ya kuruhusu matumizi ya kifaa cha mawasiliano (Type approval )
- o Leseni kwa ajili ya kuruhusu matumizi ya Namba ( Numbering Resources)



*Members of the Diplomatic Corps and other officials* .

**MAFANIKIO:**

Mfumo wa leseni wa mwingiliano wa teknolojia (Converged Licensing Framework")

Mfumo huu, ulioanzishwa mwaka 2005 umekuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya mawasliano. Kwa mfano leseni ya miundombunu, siyo tu tumeona maendeleo katika mitandao ya simu za mkononi, lakini vilevile tumeona kwa mara ya kwanza
mitandao ya mkongo baharini "Submarine cables" ikifika kwenye pwani, kwa mfano "Seacom" ambayo uliizindua 2009, na "EASSY cable" ambayo ilizinduliwa 2010.

Tumeona maendeleo mengi kwenye leseni ya matumizi (Application Service License) katika matumizi ya intanet, kutuma pesa kwa simu (M-Pesa ya Vodacom, Zap ya Airtel, Tigo-Pesa ya Tigo, Z-Pesa ya Zantel, Mobipawa ya E-fulusi). Kwa sasa ni rahisi kutulia simu ya mkononi kulipia bili za maji, umeme, DSTV nk.

Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano ya Simu Nchini

Sekta ya mawasiliano imekuwa kwa kasi sana katika kipindi kifupi. Katika miaka ya 1990 kulikuwa na kampuni moja tu ya simu. Mwaka 2000 kulikuwa na kampuni nne (4) za mitandao ya simu, na mwaka 2011 ziko 9 ambazo ni Vodacom, Airtel, Tigo, Zantel, TTCL, Benson Informatics, Sasatel, Seacom, na Six Telecoms.

Kampuni zilizokuwa zinatoa huduma (Application Service Licenses) zilikuwa 11 mwaka 2000, zikawa 23 mwaka 2005, na kufikia 68 mwaka 2010. Laini za simu zimeongezeka toka 284,109 mwaka 2000, na kuwa milioni 3.2 mwaka 2005, kufikia milioni 20.5 mwaka 2010.

Kufungua ofisi za kanda za TCRA
Mamlaka imefungua ofisi sita za kanda kwa lengo la kuwafikia wananchi kwa urahisi, kupnguza gharama za kufuata huduma makao makuu, na pia kuongeza ufanisi katika kutoa huduma. Ofisi hizi zipo Zanzibar, Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam.

**Usimamizi wa Masafa ya Mawasiliano.**
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekuwa ikutumia kwa ufanisi mitambo sita ya kisasa, pamoja na minne iliyonunuliwa mwaka 2006 ili kujiimarisha na kujiongezea uwezo wake wa kupanga na kuthibiti matumizi ya masafa nchini. Hivi sasa ofisi za Kanda ya Mamlaka ina mitambo (mobile frequency monitoring station) inayotumika kusimamia masafa. Kuwepo kwa mitambo hiyo kumepunguza muda wa kuchunguza na kumpangia muombaji masafa na kutambua kwa urahisi watumiaji haramu wa masafa na kuelewa mahali walipo; na kuzuia muingiliano (harmful interference) baina ya watumiaji wa masafa hivyo kuongeza ubora wa mawasiliano nchini.

**Usimamizi wa Namba za Simu na Uboreshaji wa Matumizi ya Namba za Dharura**
Usimamizi wa namba za mawasiliano pia umekuwa na mafanikio. Namba za simu ni moja kati ya rasilimali adimu za taifa inayotambulisha watumiaji wa simu na kuwezesha maunganisho ya simu za wateja ndani na nje ya nchi katika mitandao mbalimbali. Mamlaka imesimamia kikamilifu utekelezaji wa Mpango wa Namba wa Taifa (National Telecommunication Numbering Plan) uliopitishwa mwaka 2005/06 ili kukidhi ongezeko la wateja wa simu za mkononi. Hadi kufikia Novemba 2006 makampuni yote yalikuwa yametekeleza agizo lililowataka kubadilisha namba za mitandao yao.

Hali kadhalika, ili kuwezesha wananchi kutumia namba za dharura kikamilifu, kama 111 na 112, Mamlaka ilitenga jumla ya Shs.522 milioni kwa ajili ya kusaidia Jeshi la Polisi kujenga kituo cha kisasa cha mawasiliano ya dharura (Emergency Call Centre) kinachosimamiwa na Jeshi hilo ili kuhudumia wananchi watakaofikwa na matatizo mbali mbali. Kituo hicho kimekamilika na kina mitambo ya kisasa yenye uwezo wa kupokea simu na kutunza kumbukumbu ya simu zilizoingia hata kama haikupokelewa na kutoa taarifa ya matatizo yaliyojitokeza. Mamlaka pia ilighaamia mafunzo ya maafisa 45 wa polisi ili kuweza kutumia vifaa hivyo na kituo hiki tayari kimekabidhiwa kwa Jeshi la Polisi. Ni rai yetu kuwa kituo hicho kitatumiwa kikamilifu kwa manufaa ya wananchi wote.



*Former TCRA Content Committer Vice Chairperson Mrs. Amino Mrisho Hajjati, left and other delegates.*

**Usimamizi wa Ubora wa Vifaa vya Mawasiliano (Standards and Type Approval)**

Usimamizi wa ubora vya vifaa vya mawasiliano ni eneo jingine ambalo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inajukumu kwa mujibu wa sheria kusimamia ubora wa vifaa vya mawasiliano vinavyoaingizwa nchini na kuunganishwa na mtandao wa taifa kwa ajili ya mawasiliano mbali mbali. Lengo la kuthibiti uingizaji na usambazaji wa vifaa na vyombo vya mawasiliano ya simu na redio nchini ni kuilinda mitandao na watumiaji wa vifaa kwa kuhakikisha kuwa vifaa/vyombo husika vinakidhi viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

**Kusimamia gharama za muingiliano kati ya Makampuni ya simu nchini (Interconnection Rates).**

Kimsingi, gharama hizi ni changamoto kubwa kwa nchi zingine lakini hapa Tanzania, TCRA imefanikiwa kusimamia suala hili na kuweka viwango ambavyo hutumika na makampuni ya simu. Kabla ya mwaka 2002, viwango hivi vilikuwa ni senti 25 za kimarekani, na zilpunguzwa toka mwaka 2004. Mwaka 2008 Januari gharama hizi ziliwekwa katika kiwango cha senti 7.83 za kimarekani, mwaka 2009 senti 7.65 za kimarekani, mwaka 2010 senti 7.49 za kimarekani na mwaka huu toka Januari 1 senti 7.32 za kimarekani, ambazo ni sawa na Sh 103 za kitanzania. Kuwekwa kwa viwango hivi kumesababisha kupungua kwa gharama za simu kila mwaka.



*TCRA Officers and other delegates.*

**Mpango Mkakati (Strategic Plan)**

Mamlaka ilitengeneza mpango kabambe (Strategic Plan) kwa kipindi cha 2006/7 hadi 2010/11. Mpango huu uliweka bayana dira, dhima na vipaumbele katika kazi za Mamlaka na utekelezaji wake hatua kwa hatua.

Mpango huu ni moja ya sababu za mafanikio ya udhibiti wa sekta hii na njia inayoihakikishia Mamlaka kuwa shughuli zake mwaka hadi mwaka zinafuata utaratibu na kukidhi mahitaji ya sekta na hivyo kuweza kuisimamia sekta ya mawasiliano kwa ufanisi. Hivi sasa tuko katika mkakati wa kutengeneza tena mpango kabambe mpya wa 2011/12 hadi 2015/16 ambao uko katika hatua za mwisho kukamilika.

Uimarishaji Habari na Matumizi ya Wavuti (Internet) na Anwani Pepe zenye Kuiwakilisha Tanzania (.tz ccTLD)

Mamlaka inaendelea kuimarisha utumiaji wa intaneti ili kuhamasisha watanzania kuwa sehemu ya "Jamii habari" (information society), yaani kuwa na mfumo wa maisha ambao jamii ina fursa, haki na uwezo wa kuwasiliana, kujifunza, kupashana habari bila vikwazo kupitia "Internet". Hivi sasa kwa mujibu wa takwimu za utafiti uliofanywa na Mamlaka ya mawasiliano kuna watumiaji wa intaneti (wavuti) wapatao milioni 4.8.

Mwaka 2008 Mamlaka ilichukua hatua za makusudi na kuanzisha kituo maalum Tanzania National Information Centre (tzNIC) kwa ajili ya kusajili majina ya mitandao na anwani pepe zinazotumia jina la nchi yetu (.tz ccTLD). Matumizi ya kituo hicho yataboresha huduma hiyo na kukuza utaifa wetu.

Hali kadhalika, Mamlaka ikishirikiana na jumuiya ya watoa huduma ya intaneti (TISPA – Tanzania Internet service Providers Association) imenunua swichi za intaneti (IXPs – Internet Exchange Points) zilizowekwa kwenye miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma, na baadae Mbeya. Madhumini ya kuwekwa kwa swichi hizi ni kuwafanya watumia huduma za internet na hususani e-mail kuwasiliana kwa urahisi zaidi bila kulazimika e-mail zao kwenda katika mitandao nje ya nchi, na hivyo kupunguza gharama na kuongeza kasi ya intaneti.



*TCRA Management and other participants.*

## Usajili wa Laini za Simu

Kuanzia tarehe 1julai 2009, mamlaka ilisimamia shughuli ya usajili wa laini za simu. Kusidi la zoezi hili ni pamoja na kuwalinda wateja, kuhakikisha huduma za ziada katika huduma za simu za mkononi zinakuwa salama kwa mfano huduma za kibenki kwa kutumia simu na huduma za kulipia Ankara za huduma mbalimbali. Hali kadhalika, ilikusudiwa makampuni ya simu yaweze kuwafahamu wateja wake.

Zoezi hili limeenda vizuri na takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 80% ya laini za simu zimesajiliwa tayari, yaani laini milioni 16.5 kati ya laini 20.5 zilizopo sokoni zimesajiliwa. Haya ni mafanikio makubwa kwa nchi. Nitumie nafasi hii kuyapongeza makampuni ya simu kwa ushirikiano walioonesha katika utekelezaji wa zoezi hili. Hali kadhalika, niwapongeze watanzania waliojitokeza kwa wingi na kuitikia wito wa kusajili laini zao za simu na kuwasihi wale ambao bado hawajafanya hivyo, waharakishe na kutekeleza agizo hili kwani kwa mujibu wa sheria, ni kosa la jinai kuwa na laini ambayo haijasajiliwa.

## Sekta ya Utangazaji

Mamlaka inadhibiti sekta ya utangazaji, ambalo limeonesha mafanikio makubwa sana miaka ya karibuni. Vyombo vya Utangazaji, vikiwa ni sehemu ya Mawasiliano kwa umma ni muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla.
Tangu kufunguliwa kwa Sekta (liberalization) ya Utangazi nchini kwa wawekezaji binafsi mwaka 1993, kumekuwepo na ukuaji wa kasi kutoka radio moja tu (Radio Tanzania) hadi Radio 57 na vituo vya televisheni 29 hadi sasa. Maombi mbali mbali ya leseni za utangazaji yako katika hatua mbali mbali za mchakato wa kutoa leseni hizo kwa mujibu wa sheria.



*Part of audience and Zonal Managers.*

Mamlaka inasimamia mchakato wa mabadiliko ya mfumo wa utangazaji kutoka analojia (analogue) kwenda dijitali (digital). Mabadiliko haya yaliridhiwa na wanachama wa shirika la Mawasiliano ya Kimataifa (International Telecommunications Union – ITU) katika mkutano wao uliofanyika mjini Geneva – Uswisi June 2006. Tanzania ni mwanachama wa ITU. Mkutano huo ndio uliofikia makubaliano na kuweka taratibu ambazo zinapaswa kufuatwa na nchi zote wanachama ikiwa ni pamoja na kuanza kwa kipindi cha mpito cha urushaji wa matangazo ya digital. Mabadiliko hayo yanatakiwa yawe yamekamilika ifikapo 2015. Tanzania pamoja na nchi zingine za Afrika mashariki tumekubaliana tuwe tumekamilisha zoezi hili ifikapo 2012. Hivi sasa kuna makampuni matatu ambayo yamepewa leseni ya miondombinu (Network Facility License) ili kuwa "Multiplex Operator". Katika mfumo wa digitali, makampuni mengine yatapewa leseni ya "utangazaji" (Content Service License).
Uhamaji huu una gharama zake, ikiwemo gharama za vin'gamuzi (decoder) kwa ajili ya kunasia matangazo ambapo gharama yake inategemewa kufikia karibu dola za kimarekani 50. Tunaiomba serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia wananchi kwa kuwaondolea kodi ili wasikose huduma za utangazaji hapo itakapozimwa mitambo ya analojia inayotumika kwa sasa.

### Huduma za Posta na Simbo za Posta (Post Code).

Maendeleo ya sekta ya posta ni pamoja na ukuaji wa sekta kwa kuongeza ushindani, hususan kwenye usambazaji wa vifurushi. Mamlaka imepanga leseni tano kwa ajili ya utoaji wa huduma za nyaraka na vipeto kwa njia ya haraka (Courier Services License).

Moja kati ya hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Mawasiliano katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta (2003) ni kuibua mradi wa kuanzisha anwani mpya za kitaifa (Postcode), ambao una mfumo wa kutumia tarakimu tano (Five Digits Numerical System). Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Mh. Makamu wa Rais mwezi Januari 2010 mjini Arusha. Mradi huu unanuia kuandaa anwani ambazo zitawezesha barua na vipeto kufikishwa kwenye makazi au ofisini ya mteja ili kumpunguzia mhusika muda anaopoteza kufuata barua posta.

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano na wadau wote muhimu. Manufaa ya mfumo huu mpya wa anwani yatakuwa si kwa posta tu bali kwa jamii nzima. Utaboresha kazi za taasisi nyingine muhimu ikiwemo Polisi, Zimamoto, Mamlaka ya Mapato, Hospitali (Ambulance services), Biashara (Registration) na Uhamiaji. Vile vile utarahisha utekelezaji wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa kuwezesha bidhaa zinazonunuliwa kwa njia ya mtandao (e-commerce).




*The enthusiastics Tanzania House of Talents (THT) youth thrill the delegates.*

## Ushirikiano wa Kimataifa katika mawasiliano

Moja kati ya majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano yaliyoainishwa kwenye Sheria iliyoianzisha ni pamoja na kulipia michango kwa niaba ya serikali, kushiriki kwenye taasisi za mawasiliano za kimataifa. Mamlaka imekuwa iikilipia michango hiyo kila mwaka na kuifanya Tanzania kufaidika na huduma zitolewazo na taasisi hizo.

Taasisi za kimataifa zinazohusika kwa sasa ni pamoja na Umoja wa simu Duniani (International Telecommunication Union (ITU); Umoja wa Posta Duniani (Universal Postal Union, UPU); Umoja wa simu wa jumuia ya madola (Commonwealth Telecommunications Organisation (CTO)), Commonwealth Broadcasting Association (CBA). Kwa upande wa kontinenti la Afrika, kuna Umoja wa simu Africa (African Telecommunications Union (ATU)), Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union (PAPU)); Umoja wa Wadhibiti wa Mawasiliano Kusini mwa Afrika (CRASA), Chama cha Watangazaji Kusini mwa Afrika (SABA), Umoja wa Taasisi za Mawasiliano Afrika Mashariki (East African Communication Organisation (EACO)) na taaasisi zinginezo.

## Mawasiliano Towers.

Kwa muda mrefu sasa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilikusudia kuwa na ofisi zake za kutosheleza wafanyakazi kutoa huduma wakiwa mahali pamoja, badala ya sehemu mbili, yaani ofisi zetu zilizokuwa Upanga na Mikocheni. Jitihada zilifanyika kwa muda mrefu ili kuhakikisha kuwa azma hii inafikiwa mapema ili kuwa na ofisi nzuri zenye miundombinu mahiri ya kutekeleza majukumu ya Mamlaka hii, ikizingatiwa kukua kwa haraka kwa teknolojia katika sekta ya mawasiliano.

Kama ulivyoona wakati wa ukaguzi wa jengo hili, Idara zote za Mamlaka ziko mahala pamoja tofauti na ilivyokuwa awali ambapo zilikuwa katika majengo mawili, sehemu tofauti. Hali hiyo ilipunguza jitihada za kutoa huduma kwa ufanisi kama inavyokusudiwa. Gharama za jengo hili ni shilingi za kitanzania 39,454,028,936.

Jengo hili limejengwa na kampuni ya China Railway Jianchang Engineering (T) Co. Ltd (CRJE) kama kontrakta mkubwa, na makontrakta wadogo wa huduma, na Mshauri Mtaalamu (Consultant) ni Archplan International Inc. Lina ghorofa 14, na kwa hivi sasa ofisi zote zinatumika, ikiwa pamoja na maofisi ya TCRA, na taasisi za umma na makampuni. Vile vile, Mamlaka ina mpango wa kuanzisha makumbusho ya mawasiliano,

yaani Communication Museum katika jengo hili. Lengo ni kuweka kumbukumbu na kuhifadhi historia ya mawasiliano hapa nchini.

## CHANGAMOTO

**Gharama za huduma za mawasiliano**

Pamoja na mafanikio mazuri katika sekta ya mawasiliano, kumekuwepo na changamoto mbalimbali, kwa mfano gharama za huduma za mawasiliano ya simu na "Interneti" ingawa zimeshuka, zimebakia kuwa juu ikilinganishwa na kipato cha mwananchi. Hii kwa kiasi kikubwa imeendelea kusababishwa na kutokuwepo kwa miundo-mbinu na huduma zingine zinazohitajika katika urahisishaji wa kutoa huduma za mawasiliano.

**Kuunganisha Mawasiliano vijijini**

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni mhimili wa maendeleo ya taifa na ulimwengu kwa ujumla, mijini na vijijini. Kwa kuwa lengo kubwa la serikali ni kuwawezesha wananchi kupata Habari (universal access) na kuwa kwa njia hiyo wanachi walio wengi hawataachwa nyuma katika maendeleo ndani ya karne hii ya utandawazi, serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano itaendelea kuhakikisha kuwa rasilimali adimu zikiwemo masafa na namba za simu zinatumika kwa makini (efficiently and effectively) ili kukidhi mahitaji ya taifa na kuharakisha maendeleo. Mamlaka itandelea kuchangia katika mfuko wa mawasiliano.

**Ujenzi wa mkongo wa mawasiliano kupitia kwenye miundombinu**

Ujenzi wa mkongo wa mawasiliano (Optical fibre) unategemea upatikanaji wa vibali vya kujenga kwenye miundombinu mingine (Right of way) kama kwenye barabara, reli, njia za umeme. Mkongo wa Taifa utakapokamilika, inategemewa utapunguza kwa kiasi kikubwa huduma za mawasiliano nchini.

**Wizi wa Simu za Mkononi na miundombinu ya mawasiliano**

Kwa kipindi kirefu watumiaji na watoa huduma katika sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wameendelea kupata hasara, kutokana na wizi wa simu za mikononi na makampuni yanapata hasara kubwa kutokana na kuibiwa kwa miundo mbinu ya mawasiliano katika maeneo mbambali nchini.

Ili kupunguza na hatimaye kumaliza kabisa wizi wa simu za mkononi Mamlaka kwa kushirikiana na watoa huduma na wadhibiti wa mawasiliano Afrika Mashariki wamekubaliana kwamba kila kampuni iweke vifaa vya kutunza kumbukumbu ya simu zote zinazounganishwa na mtao wake ili wizi utokeapo wasaidie kufunga simu hiyo isiweze kuunganishwa na mtandao mwingine endapo ituzwa kwa mteja mwingine. Hili linakwenda sambamba na zoezi la uandikishaji wa laini za simu za mkononi.

Usalama katika Mtandao (Cybersecurity)

Changamoto ya usalama katika mtandao wa intaneti ni jambo la kimataifa na Tanzania kama sehemu ya jumuia ya kimataifa, haina budi kujiandaa kukabiliana nayo. Mamlaka imekuwa inajitahidi kushiriki katika mafunzo na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto hii. Aidha sheria mpya ya mawasiliano ya elektroniki na posta (EPOCA) imeainisha njia mbalimbali za kukabiliana na tatizo hili kisheria.

**Matumizi ya Intaneti kwa maendeleo**

Matumizi ya Intaneti mazuri yanaweza kuchangia katika maendeleo ya nchi katika maeneo kama Serikali Mtandao (e-Government), elimu mtandao (e-Education), afya mtandao (e-health), biashara mtandao (e-commerce) na kadhalika. Kuwepo kwa mkongo wa mawasiliano kutapelekea changamoto ya wananchi kuwa na ujuzi wa kutumia intanet kwa maendeleo.

**Uharibifu wa Mazingira**

Tokea huduma ya simu za mikononi na huduma ya kulipia kabla "Prepaid Services" zianze hapa nchini, kumekuwa na uchafufuzi mkubwa wa mazingira kwa kutupa ovyo karatasi za vocha za muda wa maongezi kila wanapomaliza kuzitumia. Aidha, betri na hata simu mbovu zimekuwa zikitupwa bila utaratibu wa kulinda mazingira. Mamlaka kwa kushirikiani na wadau mbalimbali wa Mazingira pamoja na makampuni ya simu wameweka mikakakati mbalimbali kukabiliana na tatizo hili ikiwa ni pamoja na mfumo wa kuweka fedha kwa njia ya electroniki.

**Maudhui**

Maudhui katika sekta ya Mawasiliano ni changamoto nyingine ambayo hatuna budi kukabiliana nayo ili kulinda maadili ya taifa letu. Mamlaka ina kamati ya maudhui ambayo inafuatilia kwa ufanisi changamoto zinazotokana na swala hili. Majukumu ya Kamati ni pamoja na kumshauri Waziri wa Utangazaji juu ya masuala ya kisera; kusimamia maudhui; kushughulikia malalamiko ya watumiaji na watoa huduma

## OFISI ZA MAMLAKA YA MAWASILIANO NA ANWANI

**MAKAO MAKUU**
Mawasiliano Towers
Kiwanja na. 2005/5/1, Kitalu C,
Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P 474 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2199706 - 9
+255 22 2412011/12
Nukushi: +255 22 2412009/10
Barua pepe: dg@tcra.go.tz
Tovuti: www.tcra.go.tz

### OFISI ZA KANDA

1. **KANDA ZA KASKAZINI**
Summit Centre, Ghorofa ya 3, Block B,
Barabara ya Sokoine,
S. L. P 15675, Arusha,
Simu/Nukushi +255 27 2548947,
Barua pepe: arusha@tcra.go.tz

2. **KANDA YA ZIWA**
NSSF Commercial Complex
Ghorofa ya 4, Wing B,
Barabara ya Kenyatta,
S. L. P 3108, Mwanza,
Simu/Nukushi: +255 28 2505082,
Barua pepe: mwanza@tcra@go.tz

3. **KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Century Plaza,
Plot No. 2A Block G,
Tunduma Road,
S. L. P 1375, Mbeya
Simu: +255 25 2502940,
Nukushi: +255 25 2502941,
Barua pepe: mbeya@tcra.go.tz

4. **KANDA YA KATI**
Eneo la Kisasa, Barabara ya Dar es Salaam,
Mtaa wa Natron,
S. L. P 2229, Dododma,
Simu: +255 26 23250221
Nukushi: +255 26 2350021,
Barua pepe: dodoma@tcra.go.tz

5. **KANDA YA MASHARIKI**
Mawasiliano Towers, Ghorofa ya 5
Kiwanja Na. 2005/5/1, Kitalu C,
Barabara ya Sam Nujoma.
S.L.P. 33613
Barua pepe: easternzone@tcra.go.tz

6. **ZANZIBAR**
Kiwanja S/CHR 95, Eneo la Chukwani,
S. L. P 3284, Zanzibar,
Simu/Nukushi: +255 24 2235062,
Barua pepe: zanzibar@tcra.go.tz